

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ مُحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ

SALA YA KIISLAM

Pamoja na
Tafsiri na Maelezo



SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI
AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

SALA YA KIISLAM

Mwandishi: Sheikh M. A. Durrani

© Jumuiya ya Waislaamu Waahmadiyya
Tanzania

Chapa ya mara ya kwanza Septemba 2001
Nakala 5000

Chapa ya 2023 Nakala 5000

Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waah-
madiyya Tanzania

S.L.P. 376

Dar es Salaam

Simu: +255 22 2111031

**Kimechapwa na
Ahmadiya Printing Press
S.L.P. 376
Dar es Salaam, Tanzania**

FAHARISI

Sala katika Qur'an	6
Sala katika Hadithi	8
Nyakati za Sala	9
Sharti za Sala	11
Udhu kwa picha	11
Kutanguka udhu	15
Kuvunjika sala	17
Mavazi	17
Adhana	18
Kukimu sala	23
Kukusanya sala	25
Njia ya kusali	28
Baada ya Sala	53
Rakaa za Sala	58
Sala ya Witri	59
Sala ya Ijumaa	61
Sala ya Iddi mbili	65
Sala ya Safari	67
Sala ya Tahajjud	68
Sala ya maiti	69
Sala ya Istikhara	73
Mambo kuhusu Imam	75
Sujuda Sahwi	77
Hotuba ya Nikah (Ndoa)	78
Maombi mbalimbali	82

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

UTANGULIZI

Sala ni muhimu sana katika kila dini. Katika dini ya Kiislamu Sala ni nguzo ya pili. Sala inampatia mtu nafasi ya kujitupa mbele ya Mwenyezi Mungu, kumuomba na kuongea naye. Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. alisema kwamba yeye anajipatia burudisho la macho katika sala. Siku hizi wakati watu kwa malaki wanasilimu, ni muhimu sana kuwaelemisha katika dini ya Kiislam. Kijitabu hiki kimetayarishwa kwa kipimo cha mfuko ili wanafunzi wa dini ya Kiislam waweze kukiweka katika mifuko yao na wafaidike nacho.

Katika kijitabu hiki sala za kila namna; faradhi na nafali, zimeelezwa humo, kwa matamshi na tafsiri zake. Kijitabu hiki ni ushahidi wa huduma za Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Tunamshukuru Sheikh M. A. Durrani ambaye ametutayarishia kijitabu hiki. Mwenyezi Mungu ambariki.

Jumuiya ya Waisalmu Waahmadiyya Tanzania.

SALA YA KIISLAM

Mwenyezi Mungu ametaja shabaha ya kuumbwa kwa mwanadamu kuwa ni kumwabudu Allah. Amesema kwamba:

(51:57) وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

“Na sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu mimi.” Maana ya ibada ni utiifu kamili wa maamrishi ya Mwenyezi Mungu. Katika dini ya Kiislamu ibada za aina mbalimbali zinapatikana. Kati ya nguzo tano za Kiislamu nguzo ya pili ndiyo Sala. Yaani kusali sala tano kila siku sawa na njia iliyofundishwa katika Dini. Sala ni kutoa roho moja kwa moja mbele ya Mwenyezi Mungu Mwenye enzi kwa kuamini kabisa hisani, huruma na nguvu ya Allah. Katika sala hakuna haja ya mwakilishi yeyote baina ya mtu na muumba wake.

Sala ni faradhi juu ya kila Mwislamu mwenye akili timamu na aliyebalehe. Lakini watoto wapewe mazoezi na mafunzo mapema, Ndivyo Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. alivyoagiza kwamba watoto wanapokuwa wenye umri wa

miaka saba, wazazi wawasisitize kusali. Na wasiposali katika umri wa miaka kumi wakemewe. (Abu Daudi Kitab-us-Salat).

SALA KATIKA QUR'AN TUKUFU

1. Tumehimizwa sana kusali kwa nyakati zake. Mwenyezi Mungu anasema kwamba:

إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَّقْشُورًا ﴿١٠٤﴾

Bila shaka Sala kwa waaminio ni faradhi iliyowekewa nyakati maalum (4:104).

2. Sala imelazimishwa kiasi hiki kwamba hata katika shughuli haisamehewi bali tumesisitizwa kuiangalia zaidi wakati wa shughuli mbalimbali. Mwenyezi Mungu amesema kwamba:

حُفِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَىٰ وَقُومُوا

لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٩﴾

Angalieni Sala, na hasa sala ya katikati, na simameni kwa kumnyenyekea Allah. (2:239).

Mradi wa sala ya katikati ni ile inayomkuta mtu akiwa na shughuli nyingi, na hivyo anatakiwa kuiangalia sana ili asisahau.

3. Mwenyezi Mungu ametuamuru kusali kwa faida yetu sisi. Amesema kwamba:

إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ط

Bila shaka sala huzuia mambo ya aibu na maovu (29:46).

4. Vile vile Mwenyezi Mungu amewaonya wale ambao wanaonyesha uvivu katika sala na hawadumishi sala zao. Mwenyezi Mungu amesema kwamba:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ۗ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ۗ

Basi ole kwa wanaosali; ambao wanapuuza sala zao (107:6-7).

5. Wakati mtu asiwe katika fahamu nzuri asisali mpaka atulie. Mwenyezi Mungu amesema kwamba :

لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَارَىٰ

Msiikaribie sala wakati hamna fahamu nzuri. (4:44).

(Sukaaraa haimaanishi ulevi tu bali mradi wake

ni kutofahamu kwa sababu ya njaa au hasira au usingizi au kuchoka sana n.k.).

SALA KATIKA HADITHI

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. amesema kwamba:

1. Hakika tofauti baina ya mtu na ushirikina na ukafiri ndiyo kuacha kusali (*Muslim Kitab ul-Iman baabu Tark-e- salat*).
2. Kitendo cha kwanza kitakachokaguliwa miongoni mwa vitendo vya mtu siku ya kiyama ni sala zake. Kama hesabu hiyo ikienda vyema mtu huyo atakuwa amefuzu na kufaulu. Na kama hesabu hiyo ikienda vibaya mtu huyo atakuwa ameshindwa na amepata hasara. (*Tirmidhi Kitab- us-Salat*).
3. Je mnaonaje kama kuna mto unaopita karibu na mlango wa mmoja wenu naye huyo mtu anaoga humo kila siku mara tano, Je uchafu wake wowote utabaki mwilini mwake? Masahaba wakajibu la, hautabaki uchafu wake wowote. Mtume s.a.w. akasema huo ndio mfano wa sala tano (za kila siku) ambazo kwazo Mwenyezi

Mungu anafuta makosa ya mtu.
(*Bukhari Kitabu Mawaakit us Salat*)

4. Kusali pamoja (nyuma ya Imamu) ni bora mara ishirini na saba kuliko mtu kusali peke yake.
(*Muslim Kitab-us-Salat*).

Sayyidna Ahmad a.s. amesema kwamba: Mtu ambaye hadumishi sala tano kila siku hayumo katika jamaa yangu. (*Safina ya Nuhu*).

NYAKATI ZA SALA

Mwenyezi Mungu amesema kwamba:

أَقِمِ الصَّلَاةَ لِذُنُوبِكِ الشَّمْسِ إِلَى غَسَقِ النَّيْلِ وَ
قُرْآنَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿٤٩﴾

Usimamishe sala jua linapopinduka (na jua linapopoa na jua linapopotea) mpaka giza la usiku, na kusoma Qur'an alfajiri. Hakika kusoma Qur'an alfajiri kunakubaliwa. (17:79).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu ameeleza nyakati za Sala tano za Kiislamu.

1. Sala ya Adhuhuri. Inasaliwa wakati jua linapopinduka.

2. Sala ya Alasiri inasaliwa wakati jua linaanza kupoa.
3. Sala ya Magharibi inasaliwa wakati jua linapopotea.
4. Sala ya Isha inasaliwa wakati mwanga unapopotea kabisa na giza la usiku linapoingia.
5. Sala ya Alfajiri inasaliwa Alfajiri hadi jua halijaanza kuchomoza.

Katika nyakati hizi za Sala mtu anakuwa na nafasi ya kutosha kusali mapema au kuchelewa kidogo isipokuwa wakati wa sala ya magharibi inakuwa kidogo tu.

Malaika Jibril alimuelezea Mtume s.a.w. nyakati za sala.

1. Sala ya Adhuhuri kuanzia wakati jua linapopinda mpaka kivuli cha kitu kinapokuwa sawa na kitu hicho.
2. Sala ya Alasiri kuanzia wakati kivuli cha kitu kinapokuwa sawa na kitu hicho mpaka kivuli cha kitu kinapokuwa mara mbili kuliko kitu hicho.
3. Sala ya Magharibi wakati jua linapozama.
4. Sala ya Isha kuanzia wakati wekundu wa

jua unapokwisha mpaka theluthi ya usiku.

5. Sala ya Alfajiri Kuanzia mapambazuko ya Alfajiri mpaka mwanga wa asubuhi unapoenea sana.

(Musnad Ahmad bin Hambal uk. 330/3).

SHARTI ZA SALA

Mwislamu anawajibika kutimiza sharti hizi sita kabla ya kuanza sala.

1. Wakati wa sala uwe umeingia.
2. Mwili uwe safi (pamoja na nguo).
3. Pahali pa kusalia pawe safi.
4. Mwili uwe umefunikwa vizuri wakati wa kusali
5. Kunuia sala.
6. Uso uelekee upande wa Kibla. (Katika Afrika Mashariki kibla ni upande wa Kaskazini).

UDHU

Mwenyezi Mungu ameeleza taratibu ya udhu katika Qur'an Tukufu sura ya tano; 5:7, na Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ameeleza katika Hadithi (*Bukhari Kitabu Wudhuu*).


Neno Udhu linamaanisha kuosha sehemu fulani za mwili kwa kujitayarisha kusali. Hiyo ni sharti ya Sala ambayo haina budi kutimizwa; la sivyo Sala haitasihi. Mtume Muhammad s.a.w. alifundisha kuosha viganja vya mikono mara tatu wakati wa kutawadha. Kisha mtu asukutuwe maji kinywani kwa mkono wa kulia mara tatu. Tena atie maji puani kwa mkono wa kushoto mara tatu na kuisafisha vizuri.



Kisha uso mzima uoshwe na maji mara tatu.



Kisha aoshe mikono yake mara tatu, kuanzia mkono wa kuume, hadi vikoni, viko navyo vioshwe.



Hapo uloeshe mikono na maji na upake kichwani mara moja, na pitisha kidole cha shahada cha mkono wa kuume katika sikio la kuume, na kile cha kushoto katika sikio la kushoto. Ncha za vidole hivyo zipitishwe vizuri kwa kusafisha mifuo yote ya masikio, na ziingizwe kiasi katika matundu ya masikio.



Kisha viganja vipinduliwe, na sehemu za nyuma za viganja zipitishwe kutoka nyuma ya shingo kuelekea upande wa mbele ya shingo.

Mwishowe miguu ioshwe hadi mafundoni, mafundo yakioshwa pia, mara tatu kwa kuanzia mguu wa kuume. Kama kwa sababu fulani sehemu inaoshwa mara moja moja au mbili mbili, udhu utakamilika; hata hivyo njia bora ndiyo ile tunayokuta katika sunna ya Mtume Muhammad s.a.w., yaani kuosha sehemu zote mara tatu. Basi udhu umekwisha kamilika tayari.



Inapaswa ya kwamba baada ya kutawadha dua ifuatayo isomwe:

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَّابِينَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ

Matamshi: *Allahummaj'alni minat-tawabiina waj'alni minal-mutatahiriina.*

Tafsiri: E Allah, nijaalie niwe miongoni mwa wanaotubu na nijaalie niwe miongoni mwa wanaojitakasa.

Hii ndiyo njia ya kutawadha kikawaida ambapo

mtu yu mzima, si mgonjwa na kiafya hakukatazwa kutawadha na maji. Pia ni sharti kwamba maji safi yapatikane. Kama mtu yu mgonjwa ama maji hayapo, hapo mtu anatakiwa kufanya Tayammum kwa njia ifuatayo:

Piga mikono yote miwili juu ya mahali penye vumbi safi. Kama ukiona mikono yako imeshika vumbi jingi, pulizia mbali hiyo ziada. Kisha upake mikono yako usoni. Na baada ya kupaka usoni upitisha kila kiganja kwenye sehemu za nyuma za mkono mwingine. Tayammum ndiyo mfano wa kutawadha kwa kukukumbusha kuwa ikiwezekana lazima utawadhe.

Mtu akisali, hana budi udhu wake uwe salama. Kama udhu wake haujatanguka, mtu anaweza kusali zaidi ya Sala moja kwa udhu huo huo mmoja. Hiyo yahakikisha ya kwamba lazima mtu awe na udhu pindi asalipo; siyo lazima atawadhe upya kwa kila Sala kama udhu wake haujatanguka.

MAMBO YANAYOTANGUA UDHU

- a. Kutokwa na upepo (kushuta, kujamba).
- b. Kukojoa, hata kama tone moja tu la mkojo limetoka.

- c. Kwenda haja kubwa (kunya) hata kama umetokwa na kinyesi kidogo sana.
- d. Kulala usingizi, kusinzia kiasi hiki kwamba kama hakuna kitu unachoegemea usingeweza kujizuia kuanguka.
- e. Damu ya hedhi, na pia kutokwa na manii. Hayo yamekwisha elezwa mapema.
- f. Kuhusu kutapika na kutokwa na damu, maoni yanahitilafiana. Hata hivyo mtu akijikata kidogo na kisu na kadhalika damu kidogo sana ikitoka hiyo haitaharibu udhu. Kadhalika chakula kidogo kikitoka wakati wa kuteuka haitahesabika ni matapishi. Lakini mtu akitokwa na damu au akitapika hasa atatakiwa kutawadha upya.

Mtu akivaa soksi baada ya kutawadha, hapo halazimiki kuvua soksi na kuosha miguu wakati wa kutawadha tena. Bali anapaswa tu kulowesha mikono na maji na kupaka kila mguu juu ya soksi. Ruhusa hii inaendelea hadi masaa 24 sharti asivue soksi. Msafiri anaruhusiwa kupaka juu ya soksi kwa muda wa siku tatu, usiku na mchana.

MAMBO YANAYOVUNJA SALA

Mambo yafuatayo hayalingani na usahihi wa Sala, na mtu akitenda mojawapo ya hayo Sala yake inabatilika:

1. Udhu unapotanguka.
2. Kula na kunywa mtu akiwa anasali.
3. Kuzungumza ama kumwitikia mwingine ilhali anasali.
4. Kucheka ndani ya Sala.
5. Kuelekeza uso kulia ama kushoto anaposali.

MAVAZI

Katika Sala mtu anapaswa kujifunika mwili wake vizuri, hususan uchi wake na sehemu za pembeni mwake. Wanaume wanalazimika kufunika angalau sehemu kutokea kitovu hadi magoti; magoti nayo yafunikwe. Lakini wanawake wanalazimika kufunika mwili mzima isipokuwa viganja vya mikono na miguu mpaka mafundoni. Naam, mwanamke akisali nyumbani au pamoja na wanawake wengine ambako hakuna wanaume

wanaweza kuacha wazi nyuso zao.

ADHANA

Adhana maana yake ni mwito kwenye sala inayotolewa kabla ya kila sala ya faradhi. Adhana ni ifuatayo:

اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ

Allahu Akbar (mara nne)

Allah ni Mkuu kuliko kila kitu

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Ashahadu alla ilaaha Illallaah (mara mbili)

Nashuhudia kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ ، أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ

Ashhadu anna Muhammadar-Rasuulullaah (mara mbili).

Nashuhudia kwamba Muhammad ndiye Mjumbe wa Allah.

حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ ، حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ

Hayya 'alas-Swalaah (mara mbili).

Njoooni kusali.

حَيِّ عَلَى الْفَلَّاحِ ، حَيِّ عَلَى الْفَلَّاحِ

Hayya 'alal-Falaah (mara mbili)

Njoooni kwenye ufaulu.

اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ

Allahu Akbar (mara mbili)

Allah ni Mkuu kuliko kila kitu

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Laa ilaaha illallaah.

Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

Hadhrat Umar r.a. ambaye akawa Khalifa wa Pili baadaye, pia alikuwa amekaa pamoja na Mtume s.a.w. wakati huo. Yeye alisema ya kuwa yeye naye alisikia maneno hayo hayo katika njozi yake. Hapo Mtume s.a.w. hakuwa na shaka kwamba huo ni ujumbe kutoka kwa Allah. Basi akakubali njia hiyo ya kutoa adhana ili kuwaita watu kusali msikitini. Hivyo, basi, adhana

inatambulikana duniani kote kwa njia maalum ya Waislamu kuitana kwenye Sala.

NJIA YA KUTOA ADHANA

Mwadhini, (mtoaaji adhana) anapaswa kusimama mahali palipoinuka ikiwezekana, akielekea kibla. Siku hizi kipaza sauti pia kinatumika kutoa adhana. Mwadhini anapaswa kugusa masikio yake kwa vidole vya shahada, sikio la kuume kwa kidole cha shahada cha mkono wa kuume na sikio la kushoto kwa kidole cha shahada cha mkono wa kushoto, na kutoa adhana kwa sauti ya juu. Anaposema *'Hayya Alas-Salaah'* anapaswa kugeuza kidogo uso wake upande wa kuume; na wakati wa kusema *'Hayya Alal-Falaah'* ageuze kidogo uso wake upande wa kushoto.

Katika adhana ya Sala ya Alfajiri, mwadhini anatakiwa kusema baada ya *'Hayya Alal-Falaah'* maneno yafuatayo mara mbili:

الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ

Asswalaatu khairum-minan-Naum

Sala ni bora kuliko usingizi.

Mtume s.a.w. alisema:

إِذَا سَمِعْتُمُ النَّدَاءَ فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ الْمُؤَدِّنُ

Matamshi: *Idha sami'tumun-Nida'a faquuluu mithla ma yaquulul Muadh-dhin.*

Tafsiri: Msikiapo adhan, semeni anayosema mwadhini.

Basi mtu anayesikia adhana ikitolewa anapaswa kurudia maneno ya adhana; lakini pindi mwadhini asemapo 'Hayya Alas-Salaah' na 'Hayya Alal-Falaah' hapo msikilizaji adhana aseme:

لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

Matamshi: *Laa haula wala Quwwata illaa bilaahi.*

Tafsiri: Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allah.

.. na pia mwadhini asemapo *Assalaatu khairuminan-Naum*, yeye aseme:

صَدَقْتُ وَبَرَرْتُ

Matamshi: Swaddaqa wabararta

Tafsiri: Umesema kweli na umetenda wema.

Hata kama Sala ya pamoja inasaliwa uwanjani au nje ya msikiti, adhana yapaswa kutolewa kabla ya Sala. Adhana ikiisha tolewa, msikilizaji anapaswa kuomba hivi:

اللَّهُمَّ رَبَّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ وَالصَّلَاةِ الْقَائِمَةِ
آتِ مُحَمَّدًا الْوَسِيلَةَ وَالْفَضِيلَةَ
وَأَبْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُودًا الَّذِي وَعَدْتُهُ

Matamshi: Allahumma Rabaa hadhi-hidda'watit-Taammaati wasswalaatil Qaaimati, Aati Muhammadanil Wasilata wal-fadhiilata, waddaraja-tarrafiata, wab'ath-hu maqaamam-Mahmuudanilladhii wa'attahu. Innaka laa tukhliful mi'aad.

Tafsiri: Ee Allah, Mola wa wito huu mkamilifu na Sala isimamayo, mfanye Muhammad kuwa njia (ya sisi) kukukurubia, na mpe daraja la juu na umnyanyue kwenye cheo kilichosifika ulichomwahidi. Hakika Wewe huvunji ahadi.

KUKIMU SALA

Imam anaposimama mahali pake kwa ajili ya kuongoza Sala, ndipo Ikamah inatolewa. Ikamah ni adhana kwa ufupi. Kuna baadhi ya tofauti fulani baina ya maneno ya adhana na ya Ikamah ambazo ni hizi zifuatazo.

i. Adhana inatolewa kwa sauti ya juu kabisa, lakini ikamah hutolewa kwa suati ndogo.

ii. Wakati wa kutoa ikamah vidole vya shahada haviwekwi masikioni kama inavyofanywa wakati wa kutoa adhana; bali mikono inanyoshwa tu ikining'inia kuelekea chini.

iii. Maneno Assalaatu Khairum-Minan-Naum hayatamkwi katika Ikamah ya sala ya Alfajiri.

iv. Maneno ya ikamah hutamkwa haraka haraka ambapo maneno ya adhana hutamkwa taratibu. Katika ikamah maneno haya yanaongezwa baada ya Hayya 'Alal-Falaah: Qad Qaamatis-Salaatu, Qad Qaamati-Salaah (maana yake: Sala imesimama; Sala imesimama).

v. Wakati wa kukimu (kutoa Ikamah) hugeuzi kichwa kuume na kushoto ukitamka Hayya 'Alas-Salaah na Hayya 'Alal-Falaah.

Maneno ya Ikamah ni sawa kwa Sala zote za faradhi na huwa kama ifuatavyo:

اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ
أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ
حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ
قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ
اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Matamshi: *Allahu Akbar, Allahu Akbar. Ashhadu alla ilaaha Illallaah. Ashhadu anna Muhammadar-Rasuulullaah. Hayya 'alas-Salaah. Hayya 'alal-Falaah. Qad Qaamati-Salaah, Qad Qaamati-Salaah. Allahu Akbar, Allahu Akbar. Laa ilaaha illallaah.*

Tafsiri: Allah ni Mkuu kuliko kila kitu, Allah ni Mkuu kuliko kila kitu. Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Nashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah. Njoooni kwenye Sala, njoooni kwenye ufaulu. Sala imesimama, Sala imesimama. Allah ni Mkuu kuliko kila kitu, Allah ni Mkuu kuliko kila kitu. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

Mtume Mtukufu s.a.w. aliagiza ya kwamba mwadhini ndiye atakayetoa Ikamah.

(Tirmidhi, Abwab-us-Salaat, Babu Ma Ja'a Man adh-dhana fahuwa yakiimu). Naam, haja ikipatikana, mtu mwingine anaweza kukimu akiruhusiwa na mwadhini ama Imam.

KUFUNGA NIA

Kufunga nia ni jambo la muhimu wakati wa kusali. Mwenye kusali afunge nia moyoni kwamba anasali Sala gani, ni ya faradhi ama sunna au nafali na kadhalika, na kwamba atasali rakaa ngapi. Haimlazimu kutamka maneno maalum kwa sauti ya juu. Kufunga tu nia moyoni kunatosha. Mwenye kusali pamoja na kufunga nia moyoni pia atamke Taujiih - maneno ambayo yako uk. 29.

KUKUSANYA SALA

Katika baadhi ya hali fulani Sala mbili zinaweza kukusanywa pamoja. Kwa mfano Sala ya Adhuhuri yaweza kukusanywa pamoja na Sala ya Alasiri.

kadhalika Sala ya Magharibi yaweza kukusanywa pamoja na Sala ya Isha. Masharti ya kukusanya Sala mbili ni haya yafuatayo:

- a. Kama mtu yu mgonjwa.
- b. Kama mtu yuko safarini.
- c. Kama mvua inanyesha ama inapiga dhoruba.
- d. Kama ni vigumu kufika msikitini kwa sababu ya matope na kadhalika yaliyosababishwa na mvua kubwa.
- e. Kama iko khofu fulani.
- f. Kama kuna shughuli nyingi za dini.
- g. Wakati fulani Mtume s.a.w. alikusanya sala mbili bila ya khofu wala mvua.

Ni vizuri kukusanya Sala mbili katika wakati wa Sala hiyo ya kwanza. Kwa mfano, ni afadhali kukusanya Adhuhuri na Alasiri katika wakati wa Sala ya Adhuhuri. Hata hivyo kama kuna shida, waweza kukusanya Sala mbili wakati wa Sala hiyo ya pili. Pia ujue kwamba Adhuhuri na Alasiri zaweza kukusanywa, na kadhalika Magharibi na Isha zaweza kukusanywa. Huwezi kukusanya Sala ya Alasiri na ile ya Magharibi ama Sala ya Isha na Sala ya Alfajiri, wala Sala ya Alfajiri na Adhuhuri.

Wakati wa kukusanya Sala mbili, adhana moja tu inatosha kwa Sala zote mbili, lakini ikamah itatolewa kwa kila Sala mbalimbali.

Pia ikumbukwe ya kuwa ukikusanya Sala mbili huna haja ya kusali sunna, bali Rakaa za Faradhi zinasaliwa. Naam, rakaa mbili za sunna haziachwi kabla ya Sala ya Ijumaa hata kama ukikusanya Sala ya Ijumaa na Sala ya Alasiri. Pia rakaa tatu za witri lazima zisaliwe hata ukikusanya Sala ya Magharibi na Isha.

Kama Sala mbili za Adhuhuri na Alasiri zina-kusanywa, na Imam baada ya kwisha kusalisha Adhuhuri amekwisha anza kusalisha Alasiri, hapo kama mtu anafika msikitini wala hajui kwamba Imam anasalisha Alasiri, mtu huyo aingie tu katika Sala nyuma ya Imam. Baadaye akijua kwamba Imam amesalisha Sala ya Alasiri, hapo yeye mtu huyo asali rakaa nne za Sala ya Adhuhuri, Sala ya Alasiri amekwisha sali nyuma ya Imam. Lakini aliyechelewa kufika msikitini akijua kwamba Imam anasalisha Sala ya Alasiri, mtu huyo asiungane na Imam, bali kwanza asali Sala yake ya Adhuhuri peke yake, ndipo akipata sehemu yoyote ya Alasiri nyuma ya Imam, asali naye.

Kadhalika, kama Imam anaongoza Sala ya Isha, lakini mtu aliyechelewa kufika hajui, yeye anaweza kuungana na Imam akifikiria kwamba Imam anasalisha Sala ya Magharibi. Sala yake ya Isha itasihi, na baadaye asali peke yake rakaatatu za Magharibi. Lakini akijua mapema kwamba Imam anaongoza Sala ya Isha, mtu huyo anapaswa kwanza asali Sala yake ya Magharibi peke yake ndipo aungane na Imam kusali ile sehemu iliyobakia ya Sala ya Isha. Kikawaida mtu anatakiwa kusali kwanza ile Sala iliyo ya kwanza na kisha ile ya pili.

NJIA YA KUSALI

Kikawaida Sala inapaswa kusaliwa pamoja msikitini, mahali palipotolewa kwa ibada ya Allah, lakini wakati mwingine kwa sababu fulani fulani mtu anaweza kusali mahali pengine kwa sharti mahali hapo pawe safi.

Kabla mtu hajaanza kusali, yeye anatakiwa awe safi wa mwili na awe na hakika ya kwamba nguo zake nazo ni safi. Baada ya kutawadha asimame katika safu pamoja na waaminio wengine nyuma

ya Imam, wote wakielekea Kaaba. Safu ni sharti ziwe zimenyooka, wasalio wote wasimame bega kwa bega katika safu bila mmoja wapo kumtatiza mwenzake. Mtukufu Mtume s.a.w. alisisitiza mno kunyosha safu wakati wa kusali.

Wakiisha simama katika safu nyuma ya Imam, maamuma wote wanuie kwamba wako tayari kusali Sala fulani, kisha watamke **Taujih** ifuatayo:

وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا
وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

Matamshi: *Wajjahatu wajhiya lilladhii fataras-Samawaati wal-ardha haniifan wamaa ana minal-Mushrikin.*

Tafsiri: Nimeelekeza uso wangu kwa Yule Aliyeziumba mbingu na ardhi kwa kujihalisha, nami simo miongoni mwa washirikina.

Mara kabla ya Imam kuanza kusalisha, Ikama inatolewa ambayo ni namna ya kutangaza kwamba sasa Sala inasimamishwa.


Wakati wa kusali mtu anapaswa kutia moyo kikamilifu katika Sala na kujiepusha na mawazo mengine yote.

Sala inaanzia na kutamka **Takbira Tahrira**, na njia ya kutamka Takbira tahrira ni kwamba Imam anainua mikono yake hadi kwenye ndewe za masikio yake na kutamka '*Allahu Akbar*' (Allah ni Mkuu kuliko kila kitu), na maamuma wote wanafanya hivyohivyo nyuma ya Imam.



Sawa na hadithi nyingi Mtume s.a.w. hakuinua mikono yake isipokuwa wakati wa kutamka Takbira Tahrira, yaani pindi alipoanza kusali akatamka Alahu Akbar mwanzoni mwa Rakaa ya kwanza tu pekee. Sahaba mmoja wa Mtume s.a.w., Hadhrat Abdullah Ibn Masoud r.a. anasimuliwa ya kwamba safari moja alisema:

“Hebu niwaambie namna alivyokuwa akisali Mtume s.a.w. Kisha Hadhrat Abdullah r.a. akasali na akainua mikono yake mara moja tu mwanzoni mwa Sala wakati wa kutamka Takbira Tahrira.



Baada ya kutamka Takbira Tahrima, mtu anatakiwa afunge mikono yake baina ya kifua na kitovu (mkono wa kulia ukiwa juu ya ule wa kushoto), na anatazame sehemu atakayokwenda kusujudi na kisha asome **Thanaa**; yaani kumtukuza Allah kwa maneno yafuatayo:

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ وَتَبَارَكَ اسْمُكَ
وَتَعَالَى جَدُّكَ وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ

Matamshi: *Sub-haana-kalla-humma wabi-hamdika, wa tabaara-kasmuka, wa ta'ala jadduka, walaa ilaaha ghairuka.*

Tafsiri: Utukufu ni Wako, Ee, Allah, na U pamoja na sifa zako njema. Na jina lako ni lenye mibaraka. Na shani yako iko juu. Wala hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe. (*Tirmidhi, Kitab-us-Salaat, Baabudh-Dhikri bainas-Salaati wa baina Qira'at*).

Baada ya Thanaa, inasomwa **Ta'awwudh** kimoyomoyo; ambayo ni hii:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

Matamshi: *A'udhu billahi minash-shaitaan-ir-Rajiim.*

Tafsiri: Najikinga kwa Allah katika shari ya shetani mlaaniwa.

SURA FATIHA

Kisha Imam anasoma **Bismillah** kimoyomoyo ama kwa sauti, lakini maamuma lazima wasome kimoyomoyo. Bismillah yenyewe ndiyo ifuatayo:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Matamshi: *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim.*

Tafsiri: Kwa jina la Allah, mwingi wa Rehema,

mwingi wa Ukarimu.

Sawa na hadithi, Mtume s.a.w. alisoma Tasmiyah kwa sauti na wakati mwingine kimoyomoyo. Baadhi ya Waislamu, kama vile katika nchi za Kiarabu, wanasoma tasmiyah kwa sauti lakini Wahanafii na Waislamu wengine wengi wanasoma kimoyomoyo.

Kisha Imam anasoma sura **Fatiha**.

Katika Sala za Alfajiri, Magharibi na Isha Imam anasoma sura Fatiha kwa sauti ya juu, lakini katika Sala za Adhuhuri na Alasiri anaisoma kimoyomoyo. Maamuma kwa vyovyote wanaisoma kimoyomoyo. Imam anapoisoma kwa sauti ya juu, maamuma wamfuate nyuma aya kwa aya kimoyomoyo katika nafasi baina ya kila aya mbili.

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾
مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٣﴾ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٤﴾
إِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٥﴾ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ
غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٦﴾

Matamshi: *Alhamdu Lillahi Rabbil ‘Alamiin.
Ar-Rahmaanir-Rahiim. Maaliki yaumid-Diin.*

Iyyaka na'budu wa iyyaka nasta'in. Ihdinas-Swiraatal mustaqiim. Swiratalla-dhiina an'ama 'alaihim. Ghairil magh-dhuubi 'alaihim waladh-dhaalliin.

Tafsiri: Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa walimwengu. mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu, Mmiliki wa siku ya malipo. Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada. Tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale Uliowaneemesha, si ya wale Uliowakasirikia, wala ya wale waliopotea.

Wakisha maliza sura fatiha, maamuma wasema 'Amin' (kwa sauti ndogo), na maana yake ni, Ee Allah, tupokelee dua yetu.

Baada ya hapo Imam asome sehemu yoyote ya Quran Tukufu, sura ndogo ama kwa uchache aya tatu. Kwa mfano:

SURA ALKAUTHAR

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ① إِنَّا أَعْطَيْنَكَ الْكَوْثَرَ ②
فَصَلِّ لِرَبِّكَ ③ وَأَنْحَرْ ④ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ⑤

Matamshi: *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Inaa a'tainaakal Kauthar. Fasalli lirabbika wanhar. Inna shaaniaka huwal abtar.*

Tafsiri: Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu. Hakika Tumekupa heri nyingi. Basi usali kwa Mola wako na utoe dhabihu. Hakika adui wako atakuwa mkiwa.

SURA ALIKHLAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ①
قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ② اللَّهُ الصَّمَدُ ③
لَمْ يَلِدْ ④ وَلَمْ يُولَدْ ⑤ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ⑥

Matamshi: *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul huwallahu ahad. Alla-husswamad. Lam yalid. Walam yuulad. Walam yakullahuu kufuwan ahad.*

Tafsiri: Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu. Sema: Yeye Allah ni Mmoja, Allah Asiyehitaji, Ambaye wote wanahitaji Kwake. Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala hakuna afananaye naye hata mmoja.

SURA ALFALAQ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ۝
مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۝ وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ۝
وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ۝ وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ۝

Matamshi: *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'udhu birabbil falaq. Min sharri maa khalaq, wamin sharri ghaasiqin idha waqab, wa min sharrin Naffathaati fil 'uqad, wamin sharri hasidin idhaa hasad.*

Tafsiri: Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sema najikinga kwa Mola wa mapambazuko, (Anilinde) katika shari ya Alivyoviumba, na katika shari ya giza la usiku liingiapo, na katika shari ya wale wanaopuliza mafundoni, na katika shari ya hasidi anapohusudu.

SURA ANNAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۝
مَلِكِ النَّاسِ ۝ إِلَهِ النَّاسِ ۝ مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ۝
الَّذِي يُوسَسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ۝ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ۝

Matamshi: *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'udhu birabbin-Naas, malikin-Naas, Ilaahin-Naas; min sharril waswaasil khannaas. Alladhii yuwaswisu fii suduurin-Naas. Minal jinnati wan-Naas.*

Tafsiri: Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sema: ninajikinga kwa Mola wa watu, Mfalme wa watu, Mwabudiwa wa watu, katika shari ya wasiwasi (wa shetani) aendaye kisirisiri kwa hila, atiaye wasiwasi mioyoni mwa watu, miongoni mwa majinni na watu.

Sura hizo chache tulizoandika juu ni mifano tu. Imam anaweza kuchagua sehemu yoyote ya Quran tukufu kwa kusoma baada ya Sura Fatiha.

Imam asomapo sehemu ya Quran Tukufu, maamuma wanapaswa kusikiliza wakiwa kimya, maana Quran inaagiza:

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

Tafsiri: na Quran inaposomwa, basi isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemewa. (7:205).


Sahaba mmoja wa Mtume s.a.w., Hadhrat Ubada

bin Samit r.a., anasimulia ya kuwa safari moja Mtume s.a.w. alipokuwa akiongoza Sala ya Alfajiri aliona shida kusoma aya za Quran kwa sababu ya minong'ono nyuma yake. Mtume s.a.w. alipomaliza Sala yake akawauliza masahaba zake kwamba walikuwa wanasoma aya za Quran kumfuata yeye usomaji wake? Wakajibu, Naam: Hapo Mtume s.a.w. akasema:

Msisome aya za Quran nyuma ya Imam isipokuwa Sura Fatiha, kwani Sura Fatiha ndiyo sehemu hasa ya Sala isiyoweza kutenganishwa.

Ni jambo la muhimu kabisa ya kwamba mtu yeyote asifanye lolote la kuvuruga Sala ya wenzake. kwa hiyo, kila Mwislamu anapaswa kuzingatia hadithi hiyo ya Mtume s.a.w. hapo juu.

Akiisha kusoma sehemu ya Quran, Imam anainama kwenda katika hali ya Rukuu akitamka Takbira (Allahu Akbar). Maamuma wote wanamfuata kwenda katika Rukuu. Ndani ya Rukuu, mkono wa kuume ulibonyeze goti la kuume, na mkono wa kushoto goti la kushoto, na sehemu ya juu ya mwili kutokea kiuno hadi kichwa inyooke sawasawa.



Katika Rukuu, kila moja anapaswa kusoma **Tasbihi** ifuatayo kimoyomoyo mara tatu.

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ

Matamshi: *Subhaana Rabbiyal Adhiim.*

Tafsiri: Utukufu ni wa Mola wangu, mwenye adhama.

Kisha Imam anasimama wima akinyosha mikono yake ikining'inia chini ubavuni. Anapaoanza kusimama wima anatamka **Tasmii** kwa sauti ya juu kuwajulisha maamuma kwamba yeye amesimama wima sasa baada ya Rukuu.

Tasmii ndiyo ifuatayo:

سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ



Matamshi: *Sami'allahu liman hamidah.*

Tafsiri: Allah kamsikiliza aliyemsifu. Hapo maamuma wote wanamwitikia Imam na kusema **Tahmiid** ifuatatyo:

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ


Matamshi: *Rabbanaa walakal hamdu. Hamdan kathiran tayyiban mubaarakan fihi.*

Tafsiri: Mola wetu, ni zako sifa zote njema zilizo nyingi ambamo mna baraka.

Kusimama wima baada ya Rukuu huitwa **Qauma** inayoishia kwa kusema Tahmiid.

Hapo tena Imam anatamka Takbira na kuanguka katika sujuda. Yeye kwanza anaweka magoti yake chini, tena kichwa pia. Katika hali hii, magoti, mikono, pua na paji la uso vyapaswa kugusa chini. Paji la uso liwe chini baina ya mikono miwili;

Mikono kutokea viwiko hadi vikoni isiguse chini asilani na itenganishwe na ubavu.



Mtume s.a.w. alisema kuhusu sujuda: Mnapomsujudia Allah, mnapaswa kuweka chini mikono yenu na miguu yenu kwa njia iliyo sawa. Kwa vyovyote msitandaze chini mikono yenu jinsi atandazavyo mbwa wakati wa kukaa. (*Masnad*

Ahmad bin Hambal, Jl. 3, Uk. 279, Maktaba Islami, Beirut).

Katika hali ya sujuda, vidole vya mikono vielekee kibla. Miguu iwe chini ilhali vidole vya miguu vielekee kibla.

Katika hali ya sujuda, Tasbiih ifuatayo inasomwa kwa uchache mara tatu kimoyomoyo.

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى


Matamshi: *Subhaana Rabbiyal A'laa.*

Tafsiri: Utukufu ni wa Mola wangu Aliye juu. Sujuda ni hali ya unyenyekevu mkubwa kabisa, kujitupa na unyonge sana ambako mwenye kusali anatoa moyo wake mbele ya Allah Mwenye nguvu na kumwomba msamaha.

Izingatiwe ya kuwa Mtume s.a.w. alikataza kusoma aya za Quran katika hali ya Rukuu na Sujuda (*Muslim, Kitabus-Salat, Bab Annahyi 'an Qira'atil Quran Fil-Rukuu was-Sujuud*).

Kisha Imam anatamka Takbira tena ambapo Imam pamoja na maamuma wote wanainua

kwanza kichwa kisha mikono kutoka chini na wanaketi hali inayoitwa Jilsa. Katika Jilsa, mwenye kusali analaza mguu wake wa kushoto na kuketi juu yake ilhali mguu wa kuume umesimama lakini vidole vyake vinaelekea kibla. Viganja vya mikono vinawekwa juu ya mapaja na vidole vinaelekea kibla.



Katika hali hii
**dua baina ya
sijida mbili**
inasomwa:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَأَرْحَمْنِي وَأَهْدِنِي
وَعَافِنِي وَأَجْبِرْنِي وَأَرْزُقْنِي وَأَرْفَعْنِي

Matamshi: *Allahumma-firlii, warhamnii, wahdinii, wa ‘afinii, wajburnii, warzuqnii warfa’ni.*

Tafsiri: Ee Mola, nisamehe na nirehemu na niongoze na nilinde na balaa na ila na niungie na niruzuku na ninyanyue.

Baada ya Jilsa, Imam anawaongoza maamuma kusujudia mara ya pili kwa kutamka Takbira. Hapo tena “Subhaana Rabbiyal A’laa” husemwa mara tatu. Katika kila Rakaa huwa sujda mbili kila mara. Ukiisha maliza sujuda ya pili, Rakaa yako moja imekamilika. Sasa Imam anatamka Takbira tena na kuwaongoza maamuma kwenye hali ya kusimama wima ili kuanza kusali Rakaa ya pili kama ilivyosaliwa Rakaa ya kwanza. Lakini katika Rakaa ya pili, Thanaa na ta’awwudh hazisomwi. Thanaa na ta’awwudh husomwa katika Rakaa ya kwanza peke yake. Katika Rakaa ya Pili, Imam anasoma Sura fatiha na aya chache za Quran Tukufu na anamaliza Rakaa ya pili hadi sujuda ya pili. Baada ya sujuda ya pili hasimami alivyosimama katika Rakaa ya kwanza, bali sasa anaketi jinsi alivyoketi katika Jilsa. Kuketi huku mwishoni mwa Rakaa ya pili huitwa Qaadah.

Katika hali hiyo inasomwa *Tashah-hud* ifuatayo:


التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ
 وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ
 أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Matamshi: *Attahiyatu lillahi wasswalawatu wattayyibatu. Assalaamu alaika ayuhan-Nabiyu warahmatullahi wa barakaatuh. Assalaamu ‘alainaa wa ‘alaa ‘ibadillaahis-Swalihiin. Ashhadu allaa ilaaha illallaahu wa ash-hadu anna Muhammadan abduhuu wa Rasuuluh.*

Tafsiri: Maamkizi yote ya heshima na unyenyekevu ni kwa Allah na pia Sala zote na vyote vilivyohalisika. Salamu iwe kwako, Ewe Nabii, na rehema za Allah na baraka zake. Salamu iwe kwetu sisi na kwa watumishi wema wa Allah. Nashuhudia ya kuwa hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah. Na ninashuhudia ya kuwa Muhammad ni mtumishi wake na Mtume wake.

Izingatiwe ya kwamba asaliye asomapo Tashah-hud akifikia maneno ‘*Ash-hadu alla ilaaha*

illallaahu' anapaswa kunyosha juu kidole chake cha shahada cha mkono wa kuume na kukirudisha pindi amalizapo hayo.



Imesimuliwa katika vitabu vya Hadithi za Mtume s.a.w. ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alipokuwa anaketi katika Tashah-hud alikuwa akiweka mkono wake wa kuume juu ya goti lake akikunja vidole vyake vitatu kwa kuacha kidole cha shahada na kidole gumba, na kukinyosha juu kidole cha shahada wakati aliposoma maneno Ash-hadu allaa ilaaha illallaah, na kisha kuteremsha hicho kidole baada ya kumaliza hayo maneno na kukirudisha katika hali ya kwanza. Vidole vya mkono wa kushoto vinanyooshwa juu ya goti la kushoto.

Baada ya kwisha kusoma tashah-hud, inasomwa **Sala ya Mtume** s.a.w., pamoja na baadhi ya dua nyingine kimoyomoyo.

Sala ya Mtume ni hii:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ
كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ
اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ
كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

Matamshi: *Allahumma swalli ‘alaa Muhammadin wa ‘alaa aali Muhammadin kamaa swallaita ‘alaa Ibraahiima wa ‘alaa aali Ibraahiima, Innaka hamiidum-Majiid. Allahumma baarik ‘alaa Muhammadin wa ‘alaa aali Muhammadin kamaa baarakta ‘alaa Ibraahiima wa ‘alaa aali Ibraahiima, Innaka hamiidum-Majiid.*

Tafsiri: E Allah, msalie Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama Ulivyomsalia Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye. E Allah, mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama Ulivyombariki Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye.

Sala ya Mtume s.a.w. inafuatwa na ombi fupi ama maombi ambayo baadhi yake ndiyo yafuatayo:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

Matamshi: *Rabbanaa aatinaa fidduniya hasanatan wafil Aakhirati hasanatan. Waqinaa adhaaban-Naar.*

Tafsiri: E Mola wetu, Tujaalie wema katika dunia na wema katika akhera. Na tulinde na adhabu ya Moto.

رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ ۝
رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ۝

Matamshi: *Raabij-'alnii muqimas-Swalati wamin dhurriyyatii . Rabbanaa wa taqabal du'a. Rabbanagh-fir li wa liwalidayya walil-muminiina yauma yaqumul hisaab. (Sura Ibrahimu: 14:41-42).*

Tafsiri: E Mola wetu, nijaalie niwe mwenye

kusimamisha Sala na pia wazao wangu. Ee Mola wetu, na nipokelee dua yangu. Mola wetu, nisamehe mimi na wazazi wangu na waaminio siku ya kusimama hesabu.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهَمِّ وَالْحَزَنِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْعَجْزِ وَالْكَسَلِ
وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْجُبْنِ وَالْبُخْلِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ غَلَبَةِ الدَّيْنِ وَقَهْرِ الرِّجَالِ

Matamshi: *Allahumma innii a'udhu bika minal-hammi wal-huzni. Wa a'udhu bika minal-'ajzi wal-kasli. Wa a'udhu bikaminal-jubni wal-bukhli. Wa a'udhu bika min ghalabatid-daini wa qahrir-rijaali.*

Tafsiri: E Allah, najikinga kwako dhidi ya matatizo na huzuni. Na ninajikinga kwako dhidi ya unyonge na uzembe. Na ninajikinga kwako dhidi ya woga na ubahili. Na ninajikinga kwako dhidi ya kuelemeza na deni na ukorofi wa watu. (*Abu Dawud, Kitabus-Swalaah, Babulisti - 'dhah*).

اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا وَلَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ
فَاغْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ وَأَرْحَمْنِي إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

Matamshi: *Allahumma, innii dhalamtu nafsi dhulman kathiiiran, walaa yaghfirudh-dhunuuba illa anta. Faghfiri lii maghfiratam-min in-dika warhamnii. Innaka antal-ghafuurur-Rahiim.*

Tafsiri: E Allah, nimejidhulumu nafsi yangu sana. Wala hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe, basi nighofirie dhambi na nirehemu. Hakika Wewe ndiwe Msamehevu Mwingi wa ukarimu.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَأَعُوذُ بِكَ
مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَالِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا
وَفِتْنَةِ الْمَمَاتِ اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْمَأْثَمِ وَالْمَعْرَمِ

Matamshi: *Allahumma, inni a'udhu bika mina adhabil qabri, wa a'udhu bika min fitnatil-masihid-dajjaali, wa a'udhu bika min fitnatil-mahya wafitnatil-mamaati. Allahumma, inni a'udhu bika minalma'thami wal-maghrami.*

Tafsiri: Ee Allah, najikinga kwako dhidi ya adhabu ya kaburi, na ninajikinga kwako dhidi ya fitina ya masihi-dajjali, na ninajikinga kwako dhidi ya fitina ya uhai na fitina ya mauti. E Allah,


ninajikinga kwako dhidi ya kufanya dhambi na dhidi ya kuwa na deni.

Baada ya kusoma dua mojawapo ama zaidi katika hizo hapo Imam anatoa salamu, yaani anageuza uso wake upande wa kuume na kusema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ

Assalaamu alaikum wa Rahmatullah, maana yake salamu iwe kwenu na rehema ya Allah.

Kisha anageuza uso wake upande wa kushoto na kusema pia *Assalaamu 'alaikum wa Rahmatullaah*. Imam anatoa salamu kuonesha kwamba anamaliza Sala. Na ndivyo wanavyofanya maamuma wote pia.



Kama Sala inayosaliwa si ya Rakaa mbili bali ni ya Rakaa tatu au nne, hapo muda wa kuketi katika Qa'adah mwisho wa Rakaa ya pili, unafupishwa

na mwenye kusali atasoma hadi mwisho wa Tashahhud. Baada ya Tashahhud Imamu anasema Allahu Akbar na kusimama Qiyam kumaliza Rakaa zilizosalia kama vile alivyosalisha Rakaa ya kwanza na ya pili; huku maamuma wote wakimfuata.

Kama Sala yenyewe inayosaliwa ni ya Rakaa tatu, kama Sala ya Magharibi, hapo Imam baada ya sujuda ya pili ya Rakaa ya Tatu anaketi katika hali ya Qa'dah na anasoma Tashahhud, Sala ya Mtume s.a.w. na baadhi ya dua kimoyomoyo na anatoa Salamu kumaliza Sala yake. Maamuma wote nao wanamfuata katika mambo hayo yote.

Na kama Sala ni ya rakaa nne kama vile Sala ya Adhuhuri, Alasiri na Isha, hapo Imam hakai katika Qa'dah baada ya rakaa ya Tatu, bali akiisha fanya sujuda ya pili anasimama wima katika hali ya Qiyam akitamka Takbira ili kuanza Rakaa ya nne. Maamuma wote nao wanamfuata na kusimama wima. Rakaa ya nne inasaliwa kama Rakaa ya pili na baada ya sujuda ya pili Imam anaketi katika hali ya Qa'dah inayoitwa Qa'dah ya mwisho. Hapo anasoma Tashahhud, Sala ya Mtume s.a.w., baadhi

ya dua na anatoa salamu kulia na kushoto kama ilivyokwisha elezwa hapo juu.

Mambo yafuatayo yanafaa yazingatiwe:

- i. Kama ni Qa'dah ya mwisho, hapo baada ya Tashahhud pia usome Sala ya Mtume s.a.w. na dua nyinginezo. kama siyo Qa'dah ya mwisho, utasoma Tashahhud pekee na utainuka ukisema Allahu Akbar na kuanza Rakaa nyingine.
- ii Kama ni Sala yenye Rakaa mbili, Qa'dah baada ya Rakaa ya pili ndiyo Qa'dah ya mwisho.
- iii. Kama Sala ni ya Rakaa tatu, Qa'dah baada ya Rakaa ya tatu ndiyo Qa'dah ya mwisho.
- iv. Kama Sala ina Rakaa nne, Qa'dah baada ya rakaa ya nne ndiyo Qa'dah ya mwisho.

KUMKUMBUKA ALLAH BAADA YA KUMALIZA SALA

Kuendelea kumkumbuka Allah kwa muda kidogo baada ya kumaliza Sala kwa kusoma Tasbih na Tahmid ndiyo agizo la Quran Tukufu. Allah anasema katika sura ya 4, aya ya 104:

فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَادْكُرُوا اللَّهَ

Mkimaliza Sala basi mkumbukeni Allah.

Hiyo imethibitika kutoka sunna ya Mtume s.a.w. pia. Imesimuliwa na Hadhrat Aisha r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alikuwa anaendelea kukaa baada ya kumaliza Sala na kusoma yafuatayo:

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَلِ وَالْإِكْرَامِ

Matamshi: *Allahumma antassalaamu wa minkassalaamu tabarakta ya dhal jalaali walikraam.*

Tafsiri: E Allah u amani, Na amani ya kweli hutoka kwako. Una mibaraka ewe Mwenye Utukufu na Ukarimu. (*Sahihi Muslim, Kitabul Masaajid wa Mawadhi'us-Salaah, Baab Istihbadh-Dhikri Ba'das-salaah*).

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaamini kuinua mikono baada ya Sala haikuwa kawaida ya Mtume s.a.w. Bali desturi yake siku zote ilikuwa ni kuketi kwa muda baada ya kusali na kumkumbuka Allah pasipo kuinua mikono.

Zaidi ya dua iliyotajwa hapo juu, dua hizi zifuatazo pia alizisoma Mtume s.a.w. baada ya Sala.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ
وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ
وَلَا مُعْطِيٍّ لِمَا مَنَعْتَ وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

Matamshi: *La ilaaha illallaahu wahdahuu la shariika lahuu. Lahul mulku, wa la hul hamdu. Wa huwa alaa kulli shain qadiir.*

Allahumma laa maani'a limaa a'taita, walaa mu'tiya limaa mana'ta, walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal-jaddu

Tafsiri: Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hakuna mshirika wake. Ufalme ni wake na sifa zote njema ni zake, naye ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Ee Allah, hakuna awezaye kuzuia kile Utoacho Wewe. Wala hakuna atoaye kile Ukizuiacho. Wala shani haiwezi kumnufaisha mwenye shani dhidi yako. (*Sahihi Bukhari, Kitas-Swalaah, Baab Adh-dhikr baadas-Swalaah*).

اللَّهُمَّ اَعْنِي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ

Matamshi: *Allahumma a'inii alaa dhikrika wa shukrika wa husni ibaadatika.*

Tafsiri: Ee Allah, nisaidie niweze kukumbuka na kukushukuru na kukuabudu sana.

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ وَسَلَامٌ
عَلَى الْمُرْسَلِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Matamshi: *Subhaana Rabbika Rabbil Izzati 'aama yaswifuun. Wasalaamun 'alal-Mursaliin. Walihamdu lillaahi Rabbil 'Alamiin.*

Tafsiri: Ameepukana Mola wako, Mola mwenye enzi, na yale wanayomsifu. Na amani iwe juu ya Mitume. Na sifa zote njema zamhusu Allah, Mola wa walimwengu.

Kwa kuombwa na baadhi ya Masahaba, Mtume s.a.w. aliwaambia maneno yafuatayo kwa kumtukua Allah. Baadhi ya watu wameyachukua kama ni kawaida ya siku zote. Izingatiwe ya kwamba hilo si agizo hasa kikawaida. Basi siyo jambo la lazima sana kuyasoma mara baada ya Sala

msikitini.

سُبْحَانَ اللَّهِ ، اَلْحَمْدُ لِلَّهِ ، اَللَّهُ اَكْبَرُ

- a. ***Subhaanallah***, Utukufu ni wa Allah. Yasomwa mara 33.
- b. ***Alhamdu Lillahi***, Sifa zote njema zamhusu Allah. Yasomwa mara 33.
- c. ***Allahu Akbar***. Mungu ni Mkuu kuliko vyote. Yasomwa mara 34.

IDADI YA RAKAA ZA SALA

SALA	SUNNA KABLA	FARADHI	SUNNA BAADA	WAJIBU	NAFAL
Alfajiri	2	2	-	-	-
Adhuhuri	4	4	2	-	2
Alasiri	-	4	-	-	4 kabla ya faradhi
Magharibi	-	3	2	-	2 baada ya sunna
Isha	-	4	2	-	-
Witri	-	-	-	3	-
Idul Fitr	-	-	-	2	-
Idul Adhha	-	-	-	2	-
Tahajud	-	-	-	-	8
Istikhara	-	-	-	-	2

SALA YA WITRI

Baada ya kusali sala ya Isha na kumalizika rakaa zake mbili za sunna, inalazimu kusali rakaa zingine tatu zinazoitwa Witri.

Katika rakaa hizi za Witri, inapendeza baada ya kutoka rukuu katika rakaa za mwisho kutulia wima hali mikono imenyooka mbavuni na kusoma dua hii:

اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْتَعِينُكَ وَنَسْتَغْفِرُكَ وَنُؤْمِنُ بِكَ وَنَتَوَكَّلُ
عَلَيْكَ وَنُثْنِي عَلَيْكَ الْخَيْرَ وَنَشْكُرُكَ وَلَا نَكْفُرُكَ
وَنَخْلَعُ وَنَتْرُكُ مَنْ يَفْجُرُكَ
اللَّهُمَّ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَلَكَ نُصَلِّي وَنَسْجُدُ
وَالِيَّكَ نَسْعَى وَنَخْفِدُ وَنَرْجُوا رَحْمَتَكَ
وَنَخْشَى عَذَابَكَ إِنَّ عَذَابَكَ بِالْكَفَّارِ مُلْحِقٌ

*Allahumma inna nasta'inuka Wa nastaghfiruka
wa nu'minu bika wanatawakkalu alaika wa
nuthni' alaikalkhaira wa nashkuruka wala
nakfuruka wanakhala'u wa natruku man
yafjuruka. Allahumma Iyyaka na'budu wa laka
nuswalli wa nasjudu wa Ilaika nas'a wa nahfidhu
wa narju rahmataka wa nakhsha 'adhabaka inna
'adhabaka bilkuffari mulhik.*

Tafsiri: Ee Mola, hakika sisi tunakuomba Wewe msaada, na tunakuomba ghofira, na tunakuamini, na tunakutegemea, na tunakusifu kwa sifa njema, na tunakushukuru wala hatukukufuru, na tunajitenga na kumwacha anayekuasi. Ee Mola, Wewe tu tunakuabudu na Kwako tunaomba na tunakimbilia Kwako na tunakutumikia, na tunatumai rehema Yako na kuogopa adhabu Yako. Hakika adhabu Yako itawafikia makafiri.

Au asome dua hii:

اَللّٰهُمَّ اهْدِنِيْ فِيمَنْ هَدَيْتَ وَ عَلَيِّ فِيمَنْ عَلَّمْتَ
 وَ قَوْلِيْ فِيمَنْ نَوَّيْتَ وَ بَارِكْ لِيْ فِيمَا اَعْطَيْتَ
 وَ بِنِيْ شَرًّا مَا فَضَيْتَ اِنَّكَ تَقْضِيْ وَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْكَ
 وَ اِنَّهُ لَا يَدُلُّ مِنْ وَاٰلِكَ وَ لَا يَعْزُرُ مَنْ عَادَيْتَ
 تَبَارَكَ رَبَّنَا وَ تَعَالَيْتَ

Allahummahdini fi man hadaita, wa'afini fi man 'afaita, wa tawallani fi man tawallaita, wa barikli fi ma a'taita wa kini sharra maakadhaita, Innaka takdhi walaa yuqdhalaika; wainnahu laa yadhilla man walaita, wala ya'izzu man

adaita; tabaarakta Rabbana wa ta'alaita.

Tafsiri: Ee Mola niongoze pamoja na uliowaongoza na unisamehe pamoja na uliowasamehe, na unilee pamoja na uliowalea, na unibariki katika vile ulivyonipa, na unikinge na shari uliyoihukumu; hakika Wewe unahukumu wala huhukumiwi; hakika hadhiliki unayemfanya rafiki vala hatukuki uliyemfanya adui; U Mwenye baraka, Mola wetu, na umetukuka. (*Abu Daud Kitaab-us-Salat*)

SALA YA IJUMAA

Siku ya Ijumaa, badala ya sala ya Adhuhuri, husaliwa sala ya Ijumaa nayo in sharti hizi:

1. Lazima kila Mwislamu kukoga na kuvaa nguo nzuri na kujipaka manukato, kama akiwa nayo.
2. Wakati wa sala ya Ijumaa ni ule wa Adhuhuri.
3. Sala hii ina adhana mbili, na baada ya adhana ya pili. Imam hutoa hotuba kwa kuwafunza watu wamche Mungu na kuwaamrisha mambo mazuri na kuwakataza mabaya.
4. Kabla ya kusali, Imam hutoa hotuba mbili,

hotuba ya kwanza ni hii:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ
لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Ash-hadu alla ilaaha illallahu wahdahu la sharika lahu wa ash-hadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasuluhu, Amma baad fa a'udh billahi minash-shaitwaanir rajiim, bismillahir rahmaanir rahiim.

Tafsiri: Ninashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mtumishi Wake na Mtume Wake. Na baada ya hayo, namkimbilia Mwenyezi Mungu anilinde na shetani apigwaye mawe (afukuzwaye). Kwa jin la Mwenyezi Mungu. Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Kisha atasoma Alhamdu mpaka mwisho, kisha atasema kwa lugha waisikiayo watu ili kuwapa mawaidha. Kisha atachutama kidogo, halafu asimame na atoe hotuba hii:

الْحَمْدُ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنُؤْمِنُ بِهِ وَنَتَوَكَّلُ عَلَيْهِ
 وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ
 فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضِلَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَنَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ
 وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَنَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ عِبَادَ اللَّهِ
 رَحِمَكُمُ اللَّهُ إِنْ اللَّهُ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى
 وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ
 أَذْكُرُوا اللَّهَ يَذْكُرْكُمْ وَآدَعُوهُ يُسْتَجِبْ لَكُمْ وَذَكَرُوا اللَّهَ أَكْبُرُ

**Matamshi: Alhamdu Lillahi nahmaduhu wa
 nasta'inuhu wa nastaghfiruhu wa nu'minu bihi
 wa natawakkalu alaihi wa na'udhu billahi min
 shuruuri anfusina wa min sayyiati a'malina,
 man yahdihillahu fala mudhilla lahu, waman
 yudhlilhu fala hadiya lahu wa nash-hadu alla
 ilaaha illallahu wahdahu laa shariika lahu,
 wa nash-hadu anna Muhammadan 'abduhu,
 wa rasuuluhu. 'Ibadallahi, rahimakumullahu,
 innallaha ya'muru bil adli wal ihsaani wa iitaa**

dhilkurba wayanha anilfahshaai walmunkari walbaghyi; ya idhukum la'allakum tadhakkaru-un. Udhkurullaha yadhkurkum wad'uhu yastajib lakum, waladhik-rullahi akbar.

Tafsiri: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, tunamsifu na tunamwomba msaada na tunamwomba msamaha na tunamwamini na tunamtegemea, na tunamkimbilia Mwenyezi Mungu atulinde na shari za nafsi zetu, na atulinde na uovu wa matendo yetu; yule ambaye Mwenyezi Mungu amemwongoza hakuna wa kumpoteza, na ambaye amempoteza hakuna wa kumwongoza. Nasi twashuhudia kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah aliye pekee, hana mshirika, na pia twashuhudia kwamba Muhammad ni mtumishi Wake na mjumbe Wake. Enyi watumishi wa Mwenyezi Mungu. Mungu awarehemuni, hakika Mwenyezi Mungu anaamuru mambo ya adili na hisani na kutoa kama mtoavyo kuwapa ndugu, na anakataza mambo ya aibu na yachukizayo na uasi, anawapeni mawaidha, huenda mkakumbuka. Mkumbukeni Mwenyezi Mungu naye atawakumbukeni, na mwombeni naye

atawaitikieni, na kwa hakika kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa.

Katika Ijumaa lazima kila mtu kusikiliza hotuba, hapana kusema wala kucheza; wasikilize kwa usikivu. Ikisha hotuba, mmojawapo hukimu. Kisha husaliwa raka mbili, na imam husoma sura ya Alhamdu na sura nyingine yoyote katika raka zote mbili kwa sauti kubwa.

Kabla ya sala ya Ijumaa kuna raka nne za sunna na baada yake kuna raka mbili.

SALA ZA IDI MBILI

Idi baada ya Ramadhani inaitwa Id-ul-fitri; inayokuja siku ya kwanza ya mwezi wa Shawwal. Hii ndiyo huitwa Idi ndogo.

Idi ya pili huwa siku ya kumi ya mwezi wa Dhul Hajji. Hii inaitwa Id-ul-Adh'ha au Idi kubwa. Pengine inaitwa, Siku ya Vijungu, kwa sababu ya nyama zinazochinjwa kwa sadaka.

Iko sala ihusuyo sikukuu hizi. Sharti za sala hizi mbili ni zilezile zinazotumika kwa sala ya Ijumaa, isipokuwa hotuba katika sala hizi huja baada ya raka mbili.

Sala ya sikukuu ya Idi inianza kwa kusoma Allahu Akbar na tena kusoma Thanaa mpaka mwisbo, na halafu Allahu Akbar isomwe mara saba, moja baada ya moja, mikono ikiinuliwa mpaka sawa na masikio, na hapana dharura kusoma kitu chochote baina yake. Inapokwisha Takbira ya saba, sura ya Alhamdu inasomwa na imam, na kipande chochote katika Kurani, kwa sauti kubwa; na yeye (Imam) anamaliza rakaa ya kwanza sawa sawa na sala nyingine. Anapokwisha simama kwa ajili ya rakaa ya pili inampasa kusema Takbira ya kusimama kisha aseme zingine tano na kumaliza rakaa ya pili kama desturi. Kisha Imam anatoa hotuba inayopasa kusikilizwa vizuri. Hakuna adhana wala iqama katika sala ya idi. Takbira husomwa wakati unapokwenda kuhudhuria sala ya Idi, wakati unasubiri sala ya Idi na wakati unarejea toka katika sala ya Idi. Waila husomwa mara tatu kila baada ya sala zinazosaliwa siku ya Idi. Waislamu wanapaswa kusoma maneno yanayoitwa Takbira haya yafuatayo:

اللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُ أَكْبَرُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ
وَاللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُ أَكْبَرُ، وَاللَّهُ الْحَمْدُ

Matamshi

Allahu Akbar, Allahu Akbar

Lailaha Illallahu wallahu Akbar

Allahu Akbar walillahilhamdu.

Tafsiri: Mungu ni Mkuu kuliko wote, Mungu ni Mkuu kuliko wote, hakuna anayepasa kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Mungu ni Mkuu kuliko wote Mungu ni Mkuu kuliko wote, sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu.

SALA YA SAFARI

Katika safari sala ya faradhi yenye rakaa nne husaliwa rakaa mbili, lakini sala ya magharibi na sala ya asubuhi husaliwa sawa sawa. Na sala ya sunna katika safari haina haja, ila sunna ya sala ya asubuhi na witra baada ya isha. Na kama mtu akikaa mahali pale alipokwenda kwa siku kumi na tano, basi haifai kusali sala ya safari. Au akijua kwamba mahali pale atakwenda kukaa zaidi ya siku kumi na tano, basi yeye atasali sala kama desturi, asisali sala ya safari.

Na kama imam anasali sala ya mkazi wa mji na maamuma atasali sala ya mkazi wa mji vilevile kwa kumfuata Imam, ijapokuwa yeye ni msafiri. Na kama Imam ni msafiri atasali sala ya safari, na kama maamuma pia ni msafiri basi naye atatoa salamu baada ya raka'a mbili Imam atakapotoa salamu.

Na kama maamuma ni mkazi na Imam msafiri, hapo Imam atasali sala ya safari na atapotoa salamu maamuma asitoe bali atimize sala ya mkazi.

SALA YA TAHAJJUD

Sala hii ina raka'a nane. Wakati wake ni mwanzo wa nusu ya usiku mpaka kabla ya mapambazuko. Ni vizuri raka'a zake zisaliwe mbili mbili, ndivyo alivyokuwa akiisali Mtume s.a.w, na baada ya hizi raka'a nane asali raka'a tatu za witri. Sala ya witri husaliwa baada ya Isha na wale wasioweza kuamka usiku. Lakini kama mtu anaamka kwa ajili ya kusali Tahajjud basi asali Sala ya Witri baada ya kumaliza kusali raka'a nane za Sala ya Tahajjud.

SALA YA TARAWEH YA RAMADHAN

Sala ya Taraweh ina asili moja na sala ya Tahajjud, na kwa sababu inasaliwa mwanzo wa wakati imeitwa Taraweh. Wale wasioweza kuamka mwisho wa usiku wameruhusiwa kusali baada ya Isha; na rakaa zake ni 11 pamoja na witri.

SALA YA MAITI

Kabla hajasaliwa maiti lazima aoshwe kwa njia hii: Kwanza mkoshaji atawadhe. Kisha aanze kwa kumfumbisha maiti macho na midomo kama viko wazi; halafu kumchambisha na kumtawadhisha, kisha ndiyo kumwosha kwanza upande wa kulia, kisha wa kushoto. Maji ya kuoshea yachemshwe pamoja na majani ya mkunazi (kama ikiwezekana) kisha yapozwe kwa maji baridi, maji yakiwa baridi; au moto kidogo si vibaya. Na kumpaka mwilini karafuu maiti au kitu kinukiacho vizuri, na pia kupaka katika sanda. Sanda iwe shuka tatu: shuka ya kiunoni, ya kifurani na shuka moja ndefu ya kumfunika gubigubi. Ikiwa mwanamke zaidi ya

hizo tatu kuna shungi na kitambaa cha kufungia matiti.

Baada ya watu kutawadha kama desturi wasimame katika safu, maiti alazwe kichwa chake kikiwa kuumeni kwa Imam kisha waanze sala ya jeneza kwa kusema Allahu Akbar wafunge mikono kama desturi, wasome Thanaa na Ta'awudh na sura ya Alhamdu; kisha waseme Allahu Akbar wasome Sala ya Mtume; kisha Allahu Akbar wasome dua hii:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيِّنَا وَمَيِّتِنَا وَشَاهِدِنَا وَعَائِنَا
وَصَغِيرِنَا وَكَبِيرِنَا وَذَكَرِنَا وَأُنثَانَا
اللَّهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَاجْعَلْهُ عَلَى الْإِسْلَامِ
وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ
اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ وَلَا تَفْتِنَّا بَعْدَهُ

Allahumma-ghfir lihayyina wa mayyitina wa shahidina wa ghaibina wa saghirina wa kabirina wa dhakarina wa unthana. Allahumma man ahyaitahu minna, fa ahyihi'alal Islam, wa man

tawaffaitahu minna, fatawaffahu alal iman. Allahumma la tahirna ajrahu wala taftinna baadahu.

Tafsiri: Ee Mola wetu waghofirie wazima wetu na maiti wetu, na waonekanao wetu na wasioonekana wetu na wadogo wetu na wakubwa wetu, na wanaume wetu na wanawake wetu. Ee Mola wetu Utakayemweka hai katika sisi mweke hai juu ya Uislamu, na Utakayemfisha katika sisi Umfishe juu ya imani. Ee Mola wetu, Usituharimishie ujira wake wala Usitufitinishie baada yake.

Zingatia: Iwapo maiti ni ya mwanamke msitari wa mwisho wa dua utasomeka:

اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهَا وَلَا تَقْتِنَّا بَعْدَهَا

Matamshi: *Allahumma la tahirna ajraha wala taftinna baadaha.*

Maiti akiwa mtoto mdogo wa kiume badala ya dua hiyo asomewe dua hii:

اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ لَنَا سَلَفًا وَفُرْطًا وَذُخْرًا وَأَجْرًا وَشَافِعًا وَمُشَفِّعًا

Allahmaj' alhu lana salafan wa furutan wa dhukhran wa ajran wa shaafi'an wamushaffa'an.

Tafsiri: Ee Mola mjaalie awe kwetu mtangulizi na sababu ya kupata ujira na akiba njema na sababu ya kupata thawabu.

Na iwapo ni maiti ya mtoto wa kike itaombwa dua hii:

اللَّهُمَّ اجْعَلْهَا لَنَا سَلَفًا وَفُرْطًا وَذُخْرًا وَاجْرًا وَشَافِعَةً وَمُشَفِّعَةً

Allahmaj'alha lana salafan wa furutan wa dhukhran wa ajran wa shaafi'atan wamushaffa'atan.

Baada ya dua hizi husomwa takbira ya nne: Allahu Akbar, kisha watoe salamu kuanzia kulia na kuishia kushoto kama desturi, Kisha watamtia maiti kaburini na kumfukia hata kaburi iinuke. Kisha wamwombee ghofira na yaliyo mema.

Sala hii ya jeneza haina rukuu wala sujuda wala atahiyyatu, haina adhana wala iqama.

Talaqini, Khitma, Arubaini, ni bidaa na ni mambo yaliyo kinyume cha sunna za Mtume Muhammad s.a.w. Yeye na Masahaba zake hawakufanya hivyo. Haya ni mambo ya uzushi yaliyoanzishwa baadaye.

SALAT-UL-ISTIKHARA

Sala hii inasaliwa kwa kumwomba Allah heri na mwongozo wakati mtu anapotaka kufanya kazi muhimu sana, kama vile biashara, safari, kufunga ndoa na kadhalika. Kazi yenyewe inaweza kuwa ya kidini ama ya kimaisha. Shabaha ya Sala hii ni kumwomba Allah msaada ili mtu afaulu katika shabaha yake.

Sala ya Rakaa mbili inayosaliwa kabla ya kwenda kulala usiku. Baada ya sura Fatiha, husomwa sura Al-Kafirun, katika rakaa ya kwanza, na katika rakaa ya pili, baada ya sura fatiha, Sura Ikhlaas inasomwa. katika Qa'dah baada ya kumaliza Tashahud, Sala ya Mtume na maombi mengine, dua hii ifuatayo inaombwa kabla ya kutoa salam:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَحِيرُكَ بِعِلْمِكَ وَأَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ
وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا أَقْدِرُ وَتَعْلَمُ
وَلَا أَعْلَمُ وَأَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ اللَّهُمَّ إِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا
الْأَمْرَ خَيْرٌ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي فَاقْدِرْهُ لِي
وَيَسِّرْهُ لِي ثُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ

شَرُّ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةُ أَمْرِي فَاصْرِفْهُ عَنِّي وَاصْرِفْنِي
عَنْهُ وَأَقْدِرْ لِي الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ أَرْضِنِي بِهِ

Matamshi: *Allahumma innii astakhiiruka bi-ilmika, wa astaqdiruka bi-qudratika, wa as'aluka min fadhlikal Adhiim. Fa-innaka taqdiru wala aqdiru, wa ta'lamu walaa a'lamu, wa anta 'allaamul-ghuyuub. Allahumma inkunta ta'lamu anna hadhal-amra khairullii fidini wa ma'ashi wa aaqibati amrii, faqdirhu lii wa yassirhu lii, thumma baarik li fih. Wa inkunta ta'lam anna hadhal-amra sharrulii fii diinii wa ma'ashi wa aaqibati amri fasrifhu anni, wasrifni anhu. Waqdir liyal khaira haithu kaana, thumma ardhinii bihi.*

Tafsiri: Ee Allah, nakuomba heri kwa elimu Yako, na nakuomba uwezo kwa uwezo Wako, na ninakuomba fadhili Yako kubwa. Kwani Unaweza nami siwezi, na Unajua nami sijui, nawe U mjuzi wa mambo ya ghaibu. Ee Allah, kama katika ujuzi Wako kazi hii ndiyo heri kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, basi niwezeshe hiyo na nirahisishie hiyo, kisha itilie baraka kwa ajili yangu, na kama

katika ujuzi Wako kazi hii ndiyo shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, basi Uiweke mbali nami, na niweke mbali nayo. na Nikadirie heri popote ilipo, kisha niridhishe nayo. (*Bukhari, Kitaabud-Da'waat, Baabud-Dua indal-istikhara*).

MAMBO YANAYOMLAZIMU IMAM

1. Asikawize sala na hali nyuma yake wako maamuma labda wengine ni wagonjwa au wazee au wenye haja.

2. Rakaa mbili za faradhi ya Alfajiri na Magharibi na rakaa mbili faradhi ya Isha ni lazima zisomwe kwa sauti kubwa ya kusikilizika na rakaa zingine zote zisomwe kwa siri.

3. Na kama Imam amesahau aya au tamko lolote ni lazima maamuma amtambulishe aya aliyosahau tu: au akisahau kitendo chochote maamuma aseme *Subhaanallah* tu kwa wanaume. Na kama maamuma ni wanawake wapige kofi.

4. Na kama maamuma ni mmoja tu, basi atasimama pamoja na imam kuumeni kwake. Na kama akija mwingine basi amvute yule maamuma aliye mbele ili aje nyuma ya Imam. (Na kama maamuma amemkuta Imam hajaenda rukuu au amemkuta katika rukuu na akaipata rukuu ile, basi inahesabiwa amepata rakaa. Lakini kama kamkuta Imam kishatoka rukuu itamlazimu afuate palepale alipomkuta Imam ila asihesabu kuwa hiyo ni rakaa kwake, bali Imam atakapomaliza sala na kutoa salamu, (pande zote mbili - kulia na kushoto) maamuma huyo hatatoa salamu ila atasimama palepale kumaliza rakaa alizochelewa).

5. Ni lazima Imam awe mcha Mungu na mjuzi wa Kurani. Lakini kama wote ni sawa katika kujua Qur'an basi atakuwa Imam yule aliye mkubwa wao.

6. Na kama Imam amesahau sujuda au rukuu au nguzo yoyote kwa kuzidisha au kupunguza, basi atasujuda mara mbili kabla ya salamu na maamuma pia wasujudu. Sujuda hizi zinaitwa Sujuda za kusahau.

SUJUDA ZA KUSAHAU

Kama mtu anatenda kosa ndani ya Sala ambalo linaiathiri Sala yake, hapo anatakiwa kufanya sujuda mbili za kulirekebisha kosa hilo. Kwa mfano akiwa na shaka kwamba amesali idadi sawasawa za Rakaa ama amezipunguza ama ameziongeza, hapo atafanya sujuda mbili za kusahau.

Sujuda hizo mbili zinafanywa baada ya Tashahhud, Sala ya Mtume na maombi mengineyo katika Qa'dah ya mwisho ya Sala na kabla hajatoa salam. Imam akitamka takbira anakwenda katika sujuda ambao anasema subhaana Rabbiyal A'laa mara tatu. Kisha akitamka Takbira anakaa, na hapo anatumka Takbira tena na anafanya sujuda ya pili kama ile ya kwanza. Ndipo anatumka tena Takbira na kukaa katika Qa'dah na bila kusema chochote kingine anatoa salam kulia na kushoto kama kawaida ili kumaliza Sala yake.

Kama Imam anafanya kosa linaloweza kurekebisha na sujuda mbili za kusahau, hapo maamuma wote nao wanapaswa kufanya sujuda mbili pamoja na Imam. Lakini maamuma

mmojawapo akitenda kosa, yeye huyo maamuma hatafanya sujuda za kusahau.

Kama kuna shaka kuhusu idadi ya Rakaa zilizosaliwa, hapo kanuni ya uyakini inashikwa. Yaani kama kuna shaka kwamba umesali Rakaa tatu ama nne, hapo tatu bila shaka umesali, na shaka imo katika ile ya nne kwamba umesali ama hukusali. Hapo unatakiwa kuongeza Rakaa moja ikiwa ya nne uliyo na shaka nayo kwamba ulisali ama hapana.

HOTUBA YA NIKAH (NDOA)

Imam anasimama mbele ya watu na anasoma hutoba na aya za Qur'an tukufu zifuatazo sawa na suna ya Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.

الْحَمْدُ لِلَّهِ نَحْمَلُهُ وَ نَسْتَعِينُهُ وَ نَسْتَغْفِرُهُ
وَ نَتَوَكَّلُ عَلَيْهِ وَ نَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا
وَ مِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا ، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ
وَ مَنْ يَضِلَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ
وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا
وَنِسَاءً وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ
إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ۝

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ۝
يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ
يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ۝

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَا قَدَّمَتْ
لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ۝

Tafsiri ya Aya hizo:

Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, , na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususu kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu.

Enyi mlioamini, Mwogopeni Mwenyezi Mungu na semeni usemi ulio sawa. Atawatengenezeeni vizuri mwenendo wenu na Atawasameheni madhambi yenu; na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.

Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na mtu aangalie aliyoyatanguliza kwa ajili ya kesho, na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.

Kisha Imam anatoa nasaha kuhusu Nikah na kuhusu kuanza maisha mapya baada ya kuoana. Kisha anamuuliza baba au walii wa bibi harusi kukubali Nikah kwa kutaja kiwango cha mahari. Kisha anamuuliza Bw. Harusi vile vile. Inakuwa

vizuri kila mtu ambaye anaulizwa asimame na ajibu kwa sauti ili watu waweze kusikia jibu lake. Kisha wote wanashiriki katika maombi ya pamoja yanayoongozwa na Imamu.

MAOMBI MBALIMBALI YANAYOTUMIKA KATIKA MAISHA YA KILA SIKU

1. Dua Kabla ya Kuanza kazi yoyote njema:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Matamshi: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwingi wa ukarimu.

Zingatia: Iwapo kwa bahati mbaya mtu atasahau kutamka dua hiyo mwanzo wa kitendo atatakiwa kuitamka dua ifuatayo mara tu atakapokumbuka wakati akiendelea na kirndo hicho:

بِسْمِ اللَّهِ فِي أَوَّلِهِ وَآخِرِهِ

Matamshi: *Bismillahi awwalihi waakhrihi:*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwanzo wake na mwisho wake.

2. Dua ya kuchinja mnyama.

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُ أَكْبَرُ

Matamshi: *Bismillahi Allahu Akbar*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye mkuu kuliko kila kitu.

3. **Dua wakati wa kuanza kula:**

بِسْمِ اللَّهِ وَعَلَى بَرَكَاتِهِ اللَّهُ

Matamshi: *Bismillahi Wa'ala Barakatillah.*

Tafsiri: Kwa jina la mwenyezi Mungu na kwa baraka ya Mwenyezi Mungu.

4. **Dua baada ya kumaliza kula:**

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَطْعَمَنَا وَسَقَانَا وَجَعَلَنَا
مِنَ السُّلَمِيِّينَ
اللَّهُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ وَأَطْعِمْنِي وَأَسْقِنِي خَيْرَ أُمَّةٍ

Matamshi: *Alhamdulillah ladhii at'amana wasaqaana waj'alnaa minalmuslimiin. Allahumma baarik lii fihi waa'atmani wasaqaani khairam minhu.*

Tafsiri: Kila sifa njema zinamthibitikia Mwenyezi Mungu aliyetunyweshwa na kutulisha na kutujaalia kuwa miongoni mwa Waislamu. Ee, Mwenyezi Mungu Unibariki juu ya chakula hiki na Uninyweshe na unilische kilicho bora zaidi ya hiki.

5. Dua ya Kumwombea mwenyeji wako aliyekukaribisha au uliyemtembelea:

اللَّهُمَّ بَارِكْ لَهُمْ فِي مَا كَرَّمْتَهُمْ وَاعْفِرْ لَهُمْ وَارْحَمْهُمْ

Matamshi: *Allhuma baarik lahum fii maa razaqtahum, waghfir lahum warhamhum.*

Tafsiri: Ee Mwenyezi Mungu Uwabariki katika yale Uliyowaruzuku na Uwasamehe na Uwarehemu.

6. Dua wakati wa kuanza kulala.

Mat: اللَّهُمَّ يَا سَيِّدَ أَمْوَاتٍ وَآخِيَاءٍ waahyaa

Tafsiri: Ee. Mwenyezi Mungu kwa jina lako ninakufa na kwa jina lako ninahuika.

7. Dua baada ya kuamka kutoka usingizini

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُورُ-

Matamshi: *Alhamdulillah ladhii ahyaana ba'ada maa amataana wailahin Nushuur:*

Tafsiri: kila sifa njema zinamthibitikia Mwenyezi Mungu aliyetuhisha baada ya kutufisha na kwake ndiyo marejeo.

8. Dua wakati wa kuingia chooni.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْغُبْتِ وَالْخَبَائِثِ

Matamshi: *Allahumma Inni audhubika minalkhubuthi walkhabaaith.*

Tafsiri: Ee Mola wangu, nakimbilia Kwako nijilinde na kila uchafu na yanayochukiza.

9. Dua wakati wa kutoka chooni.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنِّي الْأَذَى وَعَمَّافِي

Matamshi: *Alhamdulillah ladhii adhhaba anni ladhaa wa'afani*

Tafsiri: Kila sifa njema zinamthibitikia Mwenyezi Mungu aliyeniondolea udhia na kunipa afya.

10. Dua baada ya kuoga au kutawadha.

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَّابِينَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ

Matamshi: *Allhumma j'alni minat tawwabiin waj'alni minalmutatwahiriin.*

Tafsiri: Ee Mwenyezi Mungu nijaalie niwe miongoni mwa wanaotubu na nijaalie niwe miongoni mwa wanaojitakasa.

11. Dua wakati wa kuingia Msikitini:

بِسْمِ اللَّهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ
اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي وَافْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ

Matamshi: *Bismillahi aswalaatu wassalaamu 'alaa Rasuuli Lahii. Allahumma ghfirlii dhunuubi waftahalii Abwaaba Rahmatika.*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu na rehema na amani ziwe juu ya mtume wa Mwenyezi Mungu. Ee, Mwenyezi Mungu nisamehe madhambi yangu na Unifungulie milango ya rehema zako.

12. Dua ya kutoka Msikitini.

بِسْمِ اللَّهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ
اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي وَافْتَحْ لِي أَبْوَابَ فَضْلِكَ

Matamshi: *Bismillahi asswalaatu wassalaamu 'alaa Rasuuli Lahii. Allahumma ghufirlii dhunuubi waftahalii Abwaaba Fadhlika.*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu na rehema na amani ziwe juu ya mtume wa Mwenyezi Mungu. Ee, Mwenyezi Mungu nisamehe madhambi yangu na Unifungulie milango ya fadhili zako.

13. Dua wakati wa kuona mwezi Mpya.

اللَّهُمَّ أَهْلَهُ عَلَيْنَا يَا آمِنُ وَالْإِيمَانِ وَالسَّلَامَةِ
وَالْإِسْلَامِ رَبِّي وَرَبُّكَ اللَّهُ -

Matamshi: *Allahumma Ahillahuu 'alainaa bil-amni wal-iimani wassalaamati wal-islamii, Rabii warabbuka Allah.*

Tafsiri: Ee Mola wetu, Utuletee (mwezi mpya) huu kwa amani na imani na uslama na Uislamu. (Ee mwezi), Mungu wangu na Mungu wako ni Allah (Mwenyezi Mungu).

14. Dua ya kufunga saumu.

وَبَصَوْمِ عِدِّي تَوَيْتُ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ

Matamshi: *Wabi swaumi ghaddin nawaitu min shahri Ramadhaani.*

Tafsiri: Nanuia kufunga saumu kesho katika mwezi wa Ramadhan.

15. Dua ya wakati wa kufuturu.

اللَّهُمَّ لَكَ صُنْتُ وَبِكَ أَمِنْتُ وَعَنَيْكَ تَوَكَّلْتُ
وَعَلَى رِزْقِكَ أَفْطَرْتُ

Matamshi: *Allahumma laka swumtu wa bika aamantu wailaika tawakaltu wa'ala rizyuka aftwartu.*

Tafsiri: Ee Mwenyezi Mungu kwa jina lako nimefunga na kwako ninaamini, na kwako ninatawakali na kwa riziki yako ninafungua.

16. Dua katika usiku wa heshima (Lailatul Qadr).

اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفْوٌ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي

Matamshi: *Allahumma innaka 'afuwu tuhubbul 'afwa fa'afuwannii*

Tafsiri: Ee Mola wangu, Wewe ni Msamehevu,

Unapenda kusamehe; basi nisamehe (dhambi zangu).

17. Dua ya wakati mume na mke wanapokutana.

بِسْمِ اللَّهِ أَرْتَهُمْ جَنِبْنَا الشَّيْطَانَ
وَجَنِبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا

Matamshi: *Bismillah, Allahumma janibna shaitwwaana wajanib shaitwaana maa razaqtanaa.*

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Ee Mwenyezi Mungu Utulinde na shetani sisi wawili na Ukilinde na shetani kile utakachoturuzuku.

18. Dua ya wakati mmoja wetu anapofariki.

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

Matamshi: *Innaa lillahi wainna Ilaihi Rajiun*

Tafsiri: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwa hakika kwake sisi ni wenye kurejea.

19. Dua ya kuingia makaburini.

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَهْلَ الْقُبُورِ يَغْفِرُ اللَّهُ لَنَا
وَلَكُمْ أَنْتُمْ سَلَفْنَا وَتَحْنُ بِالْآثَرِ

Matamshi: *Assalaamu Alaikum Yaa Ahlal qubuur, yaghfirullahu lanaa walakum. Antum salafnaa wanahnu bil athar.*

Tafsiri: Amani ya Mwenyezi Mungu iwe kwenu enyi mliolazwa katika makaburi haya. Mwenyezi Mungu atusamehe sisi na ninyi. Ninyi mmetutangulia na sisi tunafuata athari yenu.

Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe kati ya hizi zifuatazo:

1. P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam.
2. P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro.
3. P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga.
4. P. O. Box 359 Iringa. Simu 2701782.
5. P. O. Box 196, Simu: 243043 Dodoma.
6. P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea.
7. P. O. Box 10723 Arusha.
8. P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora.
9. P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma.
10. P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara.
11. P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi.
12. P. O. Box 1812 Bukoba.
13. P. O. Box 28, Simu 70 Kibiti - Rufiji.
14. P. O. Box 391 Tarime.
15. P. O. Box 605 Ifakara.
16. P. O. Box 17 Kilosa.
17. P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya.
18. P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya.
19. P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya.
20. P. O. Box 77, Simu 52 Shianda Kenya.
21. P. O. Box 552 Limbe Malawi.